

Kitabu cha kwanza cha Samweli

MAZINGIRA YA VITABU VIWILI VYA SAMWELI

Hapo mwanzo vitabu viwili vya Samweli vilikuwa kitabu kimoja, kikionyesha mfululizo wa historia ya Israeli kuanzia wakati wa Waamuzi mpaka wakati wa utawala wa Daudi. Vitabu hivyo havimtaji mwandishi wake, ingawa kuna fununu kwamba baadhi ya habari zake zilikusanywa kutokana na ripoti zilizokuwa zimeandikwa na Samweli, Nathani, Gadi, Daudi na waandishi wa kitabu cha Yasheri (1 Sam 10:25; 2 Sam 1:18; 1 Nya 27:24; 29:29).

Jina la kitabu '*Samweli*' linatokana na mtu ambaye tangu mwanzo wake alikuwa mtu maalumu, naye aliwapaka mafuta wafalme wawili ambao maisha na mambo yao yanaelezwa katika kitabu chote. Wakati wenyewe wa vitabu viwili unachukua muda wa miaka themanini hadi mia moja.

Tangu Waamuzi hadi Wafalme

Mafungu ya kwanza ya 1 Samweli yanaendelea kueleza habari za historia ya Israeli tangu wakati wa kitabu cha Waamuzi. Wakati wa Mwamuzi Eli, maisha ya Israeli ya kisiasa na kidini yalifuata mfano wa wakati wa Waamuzi, watu walipomwasi Mungu na kuanguka chini ya utawala wa mataifa ya jirani (1 Sam 2:12, 32; 3:11-13; 4:10-11, 18; taz. Amu 2:13-15). Lakini Samweli aliyekuwa mkubwa katika Waamuzi wote, alipofaulu kuwahamasisha watu kuondoa miungu yao na kumrudia BWANA, Yeye BWANA katika neema yake aliwaokoa watu wake kutoka kwa maadui zao waliokuwa wamewanyanyasa (1 Sam 7:3-6, 13, 15-17; taz. Amu 2:18; 3:9, 15).

Lakini Samweli hakuweza kuleta mabadiliko ya kudumu katika taifa. Wanawe waliomfuata kuwa Waamuzi hawakufaa, na watu walidai mpango wote wa serikali ya Waamuzi uondolewe, na badala yake iingizwe serikali ya kifalme, kama ilivyokuwa katika mataifa ya jirani yao (1 Sam 8:1-5). Matokeo yake, Sauli aliwekwa kuwa mfalme wa kwanza wa Israeli, lakini Samweli aliwaonya watu kwamba jambo hilo lisingeondoa matatizo ya taifa. Chini ya Waamuzi Waisraeli waliadhibiwa kwa ajili ya kuasi na kutokuamini kwao (1 Sam 12:9-11), na chini ya wafalme wangedhibiwa kwa sababu hizo hizo (1 Sam 12:13-15).

Wakati wa kwanza wa ufalme wa Israeli mambo mengi ya utawala yalifanana na ule wa Waamuzi. Hayo yalionekana hasa kwa jinsi viongozi walivyopewa nguvu maalumu ya Roho wa Mungu, ili waweze kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa watawala wa kigeni, na kutimiza kazi nyingine walizopewa (1 Sam 10:6; 11:6, 11; taz. Amu 3:10; 6:34; 11:29; 14:6, 19). Hivyo Sauli alipomwasi Mungu na kukataliwa, Roho wa Mungu alimtoka naye akaja juu ya Daudi (1 Sam 16:13-14).

Lakini Daudi alikuwa kiongozi wa mwisho aliyepewa Roho wa Mungu. Watu walitaka, na walipewa mpango wa serikali isiyokuwa na haja tena ya viongozi wa namna hiyo. Baada ya kuimarishwa kwa ufalme sawa sawa, uongozi siku zote ungekabidhiwa au kurithiwa kutoka kwa baba hadi mwanawe (1 Sam 8:19-22)

Kinyume cha Sauli, Daudi alijinyenyekeza mbele ya Mungu, naye alitamani kutimiza mapenzi yake (Zab 89:20; Mdo 13:22). Kwa Daudi wakati mpya kabisa ulianza, na hatimaye Waisraeli waliimarika kitaifa na kufanikiwa, kama walivyokuwa wametamani kwa muda mrefu. Baada ya hayo, vitabu vya Samweli vinaeleza habari za utawala wa Daudi ambaye, katika nyakati zote zilizofuata, alihesabiwa kuwa mfalme mkuu wa Israeli, na mzazi mkuu wa Masihi aliyehidiwa (2 Sam 7:12-16; Mt 22:42; Lk 1:32-33).

MUHTASARI WA 1 SAMWELI

1:1-7:17	Israeli chini ya Eli na Samweli
8:1-12:25	Kuanzishwa kwa ufalme
13:1-15:35	Ushindi wa kwanza wa Sauli
16:1-19:24	Kuinuka kwa Daudi
20:1-31:13	Sauli amwudhi Daudi